HISTORIA YA PAROKIA YA MT. MARTIN DE PORRES MWANANYAMALA

Utangulizi

Kabla ya kuanzishwa kituo cha sala Kinondoni(Shule ya Msingi Kinondoni) na kuwa Kigango cha Mwananyamala na baadaye Parokia ya Mt. Martin De Porres Mwananyamala, waumini wa maeneo ya Kinondoni, Kinondoni shamba, Hananasif, Mwananyamala, Kijitonyama na Mwenge, Mwananyamala Kisiwani na Top Life walikuwa wanakwenda kusali kwenye Parokia za Oystarbey, St Joseph, Kawe na Magomeni.Chini ya muongozo wa Kanisa Kuu la St Joseph Carhedral walimteua **Padri Denis** asimamie kituo cha sala cha Kinodnoni, ilikuwa mwaka 1964. Padri Denis aliyekuwa Paroko wa Oystarbey na Kituo cha sala cha Kinondoni kilikuwa chini ya usimamizi wa Parokia ya Oystarbey kuanzia kituo cha sala kianzishwe hadi kuwa Parokia mwaka 1971.Sasa hivi Parokia hii ina jumla ya Kanda Kumi na mbili(12) na Jumuiya Sabini na Tisa (79) na Jumla ya waumini ni **Elfu Kumi na mbili mia nane kumi na mbili (12,812).**

Kuanzishwa kituo cha Sala Kinondoni.

Mwaka 1964 Uongozi wa Oystarbey wakishirikiana na Padri Denis walianzisha kituo cha sala Kinondoni. Kituo hiki kilikuwa kinawahudumia wamumini wa maeneo ya Kinondoni, Kinondoni Shamba, Hanansifu, Mwananyamala, Mwananyamala Kisiwani, Kijitonyama na Mwenge. Idadi kamili ya waumini haikujulikana ilikadiliwa kuwa na waumini 200. Kituo hiki cha sala kiliendelea kwa muda wa miaka Minne(4) mwaka 1968 kituo kilipandishwa hadhi kuwa Kigango.

Kubadilisha Jina la Kigango cha Kinondoni na kuwa Kigango cha Mwanayamala

Mwaka 1968 kilipatikana kiwanja maeneo ya Mwananyamala kwa ajili ya kujenga Kigango ili waumini wahamie katika majengo yao. Kigango cha Kinondoni kilikuwa kinatumia majengo ya shule ya msingi Kinondoni

(Ukumbi wa Kulia chakula). Uongozi wa baraza au Kamati iliyoteuliwa kutoka Parokia ya Oystarbey ambayo wajumbe wake walikuwa wajumbe wa kamati ya Parokia ya Oystarbey walifanya kazi ya kuhamasisha waumini ili kuanza kusali katika kituo cha sala Kinondoni.

Mwaka 1970 ujenzi wa jengo la Kigango cha Mwananyamala ulikamlika, waumini waliombwa wahamie katika majengo yao na kubadilisha jina la Kigango kutoka Kinondoni na kuwa **Kigango cha Mwananyamala**. Idadi ya waumini iliongezeka na kufikia hadi 300. Padri aliyekuwa anawahudumia kwenye Kigango hiki ni Padri wa Shirika la White Fathers Padri Simits, pia Padre Novatus Paroko wa St Joseph na Padri Manswetu nao walikuwa wakija kutoa huduma.

Kigango cha Mwananyamala kuwa Parokia

Ujenzi wa Kanisa ulipomalizika pamoja na nyumba ndogo ya mapadri ambao ipo katika maeneo ya nyumba ya masista ndipo wakafika mapadri wa Utume wa Benedictini kutoka Jimbo la Songea ambao ni **Padri Paul Dirmin Rudmanni ambaye ndiye Paroko wa kwanza akisaidiana na Padri Primin, mwaka 1971**. Msimamizi wa Parokia ni Mt. Martin De Porres. Mapadri hawa waliishi kwa muda wa mwaka mmoja na kuondoka kuelekea Kenya.

Mwaka 1972 aliletwa Padri Guntrane kutoka Songea wa shirika la Benedictin, mipango ya Padre huyo ilikuwa kuongeza maeneo ya Kanisa ili kuwe na eneo la kutosha ili ajenge Hostel, Kituo cha Afya na Ufundi. Bahati mbaya afya ya Padri Guntrane haikuwa nzuri akalazimika kuondoka kwenda kwao Ujerumani, Novemba 1972.

Mwaka 1973 alitumwa Padre Maurus ambaye siku ya Jumapili moja alijitambulisha mwenyewe ndiye Paroko wa Parokia ya Mt. Martin De Porres Mwananyamala anachukua nafasi ya Padri aliyerudi kwao

Ujerumain naye alitokea Jimbo Katoliki la Songea pia Padri Andellehem kutoka songea naye alikuja kusaidiana na Paroko.

Mapadri hawa walifanya kazi ya kusimamia ujenzi wa ukumbi wa Parokia (Parish Hall), Mapadri hawa walifanya kazi nzuri sana na walifanikiwa kujenga majengo ambayo baadaye yalifanywa kuwa Kigango cha Mwengepia walijenga numba za masista Mwananyamala na Mwenge.Kanisa liliendelea kustawi kwa haraka sana na waumini waliongezeka na kukawa na Misa mbili.

Unzishwaji wa Kigango cha Mwenge

Kufikia mwaka 1977 Mapadri hawa, Padre Maurus na Padre Abdleherm walianzisha ujenzi wa Kigango cha Mwenge pia walijenga nyumba ya masista.Mapadri hawa wa utume wa Benedictin Fathers walifanya kazi kubwa sana na waumini waliongezeka waliagiza Kengele kubwa na kujenga Mnara wa Kengele baada ya kazi hiyo waliondoka na Utawa huo haukurudi tena.

Ujio wa Mapadri wa Shirika la mapadri waeupe (White Fathers)

Baada ya mapadri wa shirika la wabedictin kuondoka June 1979 walikuja mapadri wa Shirika la White fathers wao walikaa kwa muda maalumu wa mwaka mmoja kama walivyoangizwa na Jimbo kwa kazi maalumu ya kufanya maandalizi ya ujenzi wa Parokia ya Manzese. Mapadri hao ni Padri Nroff aliyekuwa Paroko, Padri Matter na Padri Benard. Mapadri hawa pamoja na kukaa kwa muda mfupi waliweza kuwahamasisha waumini kutoa sadaka kwa moyo wa Upendo. Waumini walianza kutoa sadaka kutoka **senti kumi hadi kufikia senti 50**, walichora mchoro kuonyesha mipaka ya eneo moja hadi jingine.

Ujio wa Mapadri wa Shirika la Consolata Fathers

Mwezi July 1979 walifika Mapadri wa shirika la Consolata Fathers kutoka Iringa na kuanza utume katika Parokia ya Mt Martin De Porres Mwananyamala. Mapadri hawa waliimarisha Vikundi vidogo vidogo(Sasa hii ni Jumuiya) Katika Maeneo yote pia waliimarisha na Jumuiya za Parokia(sasa hivi ni Kanda) Mpango huo uliweza kuwaibua wakristo wengi Mitaani na kuweza kufahamiana . Mapadri hawa waliteua Viongozi wa Vikundi mbalimba (Sasa hivi ni Jumuiya) Mapadri hao ni Padri John Bletera Paroko, alifuata Padri Jones Mario, Padri Thomas Gomes, Padri Aloyce Akossato na Padri John Berthello.

Kuanzishwa Kigango cha Hananasif

Mwanzoni mwa Mwaka 1982 ujenzi wa kituo cha maendeleo cha Mtakatifu Anna, St Anne's Multipurpose Centre ulianza kwa kusimamiwa na Paroko wa Parokia ya Mt Martin De Porres Mwananyamala Padri Thomas. Kazi hiyo iliendelea vizuri, baada ya kazi nzuri ya kupata kiwanja iliyofanywa na Padri Berthello ambaye alishirikiana kwa karibu na Kamati Tendaji ya Parokia pamoja na waumini wa maeneo hayo. Kituo hiki kilifunguliwa na mwadhama Kadinali Laurean Rugambwa tarehe 31/05/1987 wakati huo mwenyekiti wa Parokia alikuwa ndugu Marcus Mzalia baadaye waumini wakawa wanasali katika kituo hicho, kikawa kigango na hatimaye sasa hivi ni Parokia ya Hananasif.

Mwezi **August 1982** alipofika Padre Joseph De Dominicus asiye na shirika maalumu kutoka Burundi, akitokea Iringa akiambatana na Padri Angelo Pizzala yeye alikuwa wa shirika la Consolata Mapadri hawa walifanya kazi nzuri sana ya kuhamasisha waumini kujiunga kwenye vikundi ambavyo wenyewe walivipa majina kutokana na Jiografia ya maeneo husika.Mfano Kikundi cha Mchangani maeneo hayo kulikuwa na mchanga mwingi, Kikundi cha mbuyuni(Kulikuwa na mbuyu mkubwa)kikundi cha msikitini(Kulikuwa na msikiti maeneo hayo.

Mapadri hawa walifanya kazi ya kuvitembelea Vikundi na kuteua Wenyekiti na Makatibu na walijipangia ratiba ya kivitembelea vikundi na kusali na waumini.Idadi ya waumini iliongezeka mara dufu kwenda kusali kanisani.Uongozi wa Jimbo uliwapongeza mapadri hao na kuwa Parokia ya kuigwa.Vikundi hivi vilidumu na kushamili sana.Waliunganisha vikundi kadha na kuitwa jumuiya ya Mwananyamala, Kinondoni, Kisiwani kulingana na maeneo husika. Hadi shirika hilo linaondoka katika Parokia ya Mwanayamala vikundi hivi na jumuiya vilileta maendeleo ya Kiroho.Huduma mbalimbali za kiroho kama kuandikishwa watoto wa Ubatizo, taarifa za misiba, ilikuwa lazima ziletwe Parokiani na Viongozi wa Vikundi na Jumuiya.

Ujio wa Shirika la Kazi ya Roho Mtakatifu

Baada ya shirika la Wakoslolata kuondoka Mwezi **January 1989** waliwasili mapadri wa shirika la Kazi ya Roho Mtakatifu. Paroko wa kwanza kwa shirika hilo ni **Padri Plato Tarimo** na Paroko msaidizi ni **Padri Thadei Mshanga**.Mapadri hawa walifanya kazi nzuri kwa kuhamasisha kubadili majina ya vikundi na kuita majina ambayo angalau yanaleta maana badala ya kuwa na kikundi kinachoitwa Mbuyuni, Mchangani, magharibi n.k.Waumini walianza kubadili majina ya vikundi hivi na kuviita mfano; Upendo au Kikundi cha Mt Maria, Mt Yohana Mbatizaji n.k

Kubadilisha majina ya Vikundi na kuwa Jumuiya na Jumuiya kuwa Kanda.

Ujio wa Mapadri hawa wa shirika la Kazi ya Roho Mtakatifu walileta maboresho ya kubadilisha majina kutoka kikundi na kuwa Jumuiya na Kutoka Jumuiya na kuwa Kanda.Mabadiliko hayo yalileta uhai sana kwenye Jumuiya na kubadilisha uwakilishi katika Baraza la walei.

Mwanzo uwakilishi au uundaji wa Baraza la walei Parokia ilikuwa ni kila Kiongozi wa Kikundi na baadaye ikawa kila viongozi wawili wa Jumuiya yaani mwenyekiti na Katibu na baadaye ikawa Viongozi wawili wa Kanda

na wajumbe watato(5) walioteuliwa na Paroko, hao walikuwa wanaunda Baraza la walei ngazi ya Parokia. Utaratibu huo wa kuondoa jina la Kikundi na kuwa Jumuiya na kutoka Jumuiya na kuwa Kanda ulileta hamasa sana kwa waamini. Waamini kwenye jumuiya zao walibadili majina ya jumuiya na kuita majina ya Watakatifu mbalimbali.

Upanuzi wa Kanisa na Ujenzi wa Groto la Mama Bikira Maria

Mwaka 1991 Idadi ya waamini iliongezeka sana baada ya kazi nzuri ya Mapadri wa shirika la kazi ya Roho Mtakatifu ya kuwahamasisha waumini kusali.Uhamasishaji huu ulifanyika wakati wa kutembelea Jumuiya na Kanda na mahubiri mbalimbali yaliyofanywa na Mapadri kanisani. Chini ya Uongozi wa Baba Paroko Plato Tarimo akishirikiana na Viongozi wa Halmashauri ya walei waliwahamasisha waumini kuchangia upanuzi wa kanisa na ujenzi wa Groto la Mama Bikira Maria, Kazi hiyo ilifanyika kwa ufanisi mkubwa.Upanuzi wa kanisa na ujezi wa Groto ulimalizika haraka sana.Waamini walipongeza sana juhudi zilizofanywa na Paroko na Uongozi wa Halmashauri ya Walei.

Mwezi **April 1993** Padri Plato Tarimo alihama na nafasi yake kuchukuliwa na Padre Thadei Mshanga naye aliendeleza kazi njema iliyoachwa na watangulizi wake akisaidiana na Padri A.Kimario, baadaye alikuja Paroko mwingine ambaye ni Padri Macha.Paroko huyu hakukaa kwa muda mrefu katika Parokia hii alihamishwa na kuletwa Paroko mwingine.

Mwezi February 1996 aliwasili Padri Benedict Ndeyekiyo kuwa Paroko wa Parokia ya Mt Martin De Pores Mwananyamala akiwa na Paroko msaidizi Padri Priscus Jumamosi. Paroko Benedict Ndeyekiyo alifufua kwa kasi kubwa ushiriki wa waumini kwenye Jumuiya, kanda na ustawi wa waamini katika Parokia hii.Aliweza kuweka utaratibu wa kila Jumuiya wapangiwe siku maalumu ya kuadhimisha Misa. Kila jumuiya isome Misa angalau mara moja kwa mwaka ili iamshe Imani kwa wakristo.Pia alianzisha Utaratibu wa kuzitembelea familia za wakristo wote waliopo kwenye Parokia.Alikwenda

nyumba kwa nyumba, chumba kwa chumba kwa wakristo waliopanga.Utaratibu huu uliwashangaza sana waumini kwa Padri kutembelea nyumba za wakristo na kuzibariki.

Kuanzishwa kituo cha sala katika shule ya msingi Kijitonyama Kisiwani

Paroko Benedict Ndeyekiyo baada ya kuona idadi ya waamini imeongezeka sana alianzisha kituo cha sala kitumike kuendesha Ibada ya Misa kila Jumapili. Kwa ushirikiano wa viongozi wa Halmashauri ya Walei pamoja viongozi wa kanda zilizopo kijitonyama walifanikiwa kupata eneo ambalo limo ndani ya shule ya msingi Kijitonyama Kisiwani waumini wakawa wanasali katika majengo ya shule hiyo hadi walipopata eneo linguine.

January 1999 Paroko Padri Benedict alipata uhamisho na kwenda Marekani. Kwa mara ya kwanza waumini wa Parokia ya Mwananyamala waliamua kumfanyia sherehe kubwa sana na kumpa zawadi mbalimbali kwa kazi kubwa aliyoifanya ikiwa ni shukrani kwa Mungu kwa kumtumia vyema Mtumishi wake. Aliyekuwa msaidizi wake Padri Priscus Jumamosi, akawa Paroko akisaidiana na Padri Thomas Bujiku, na Padri Ernest

Paroko Padri Priscus Jumamaosi naye aliendeleza kazi nzuri iliyoachwa na mtangulizi wake kwa ushirikiano mzuri na Halmashauri ya walei pamoja na waamini kwa ujumla.

Ujenzi wa Uzio wa Eneo la Kanisa

Baba Paroko Priscus Jumamosi kwa ushirikiano wa Halmashauri ya Walei Parokia walihamasisha michango kutoka kwa waumini ili ujengwe uzio wa eneo la Parokia ambalo lilikuwa limepandwa Miti ya michongoma.Uzio huo wa matofali pamoja na nondo ulijengwa na kubadilisha madhari ya Parokia lakini pia kwa usalama wa maeneo yote ya kanisa.Paroko Priscus Jumamosi pia alianzisha shule ya mafunzo ya Computer kwa waumini na hata kwa watu mbalimbali waliopenda. Shule hiyo ilidumu kwa muda wa

mwaka mmoja na nusu.Baada ya kushindwa kujiendesha kwa faida iliamuliwa kufungwa, pia Padre Ndekumanya na Padri Gasper walihudumu katika Parokia.

Mwaka 2003 Paroko Priscus Jumamosi alichaguliwa kujiunga na chuo Kikuu cha Dar es salaama kwa masomo. Aliletwa Paroko mwingine ambaye ni **Padri Thadeius Mworia**, akisaidiana na Padri Ndekumanya na baadaye Padri Ndekumanya alihamishiwa morogoro kwenye chuo kinachosimamiwa na Shirika lao na kuletwa Paroko Msaidizi Padri Ernest.

Paroko Thadeius Moria alifanya kazi nzuri sana ya kuimarisha imani ya Wakirsto katika Parokia hii kazi aliyoifanya kwa ushirikiano na Halmashauri ya walei Parokia kwa kusimamia michango na kuhamasisha utoaji ili kituo cha sala kilichopo katika shule ya msingi Kijitonyama Kisiwani kiendelezwe kwa sababu serikali ilitoa agizo kuwa madhehebu yote ya dini yahame kwenye majengo ya shule ambayo yanafanyia Ibada.

Kwa usimaizi wa Paroko Thadeus Mworia kilipatikana kiwanja jirani na shule hiyo na alihamasisha kiwanja hicho kinunuliwe. Kiwanja hicho kilinunuliwa.Waamini wa Parokia pamoja na wale wa kituo cha sala Kijitonyama walijenga Banda la Muda na kuhamia katika eneo hilo.Michango iliendelea kwa kasi ili kuendelea kununua maeneo mengine ili kuwe na eneo kubwa.Mpaka Paroko Mworia anahama michango ya ununuzi wa viwanja ulikuwa unaendelea.

Mwaka 2007 Novemba aliletwa Paroko mwingine ambaye ni **Padri Phocas Massawe** akisaidiwa na Paroko Msaidizi Padri Ndekumanya.Paroko huyu alifanya kazi nzuri sana ya kuendeleza yale yaliyoachwa na mtangulizi wake. Aliwekeza nguvu zake zote kwa usimamizi wa ununuzi wa Viwanja katika kituo cha sala Kijitonyama. Kwa usimamizi wake vilinunuliwa viwanja sita(6) pia katika usimamimizi wake kituo cha sala **kilipandishwa hadhi na**

kuwa kigango. Na aliwahamasisha waumini kuchangia ujenzi wa nyumba ya Padre ambayo ilijengwa nyumba nzuri ya grorofa moja. Kwa sasa kigango hicho ni **Parokia ya Mt. Yakobo Mtume**. Padri Ndekumanya alihamishwa na aliletwa Paroko msaidizi Padre Robert Makanja naye baada ya muda alihamishiwa Ujerumani Akaletwa Paroko msaidizi Padri John Minde ambaye nae baada ya muda alihamishwa kwenda Marekani. Akaletwa Paroko Msaidizi Padri Arnold Babu. Baada ya kigango Cha Mt. Yakobo mtume kuwa Parokia Padre Arnold Babu aliteuliwa kuwa Paroko wa Parokia hiyo. Aliletwa Paroko Msaidizi mwingine Padri Denis Ssebuffu alifanya kazi.

Uwekaji wa Vigae(tiles) ndani ya kanisa naVitofali(Paving Blocks) maeneo yote ya Kanisa

Paroko Phocas Massawe kwa kushirikiana na Viongozi wa Halmashauri ya walei na waumini kwa Ujumla alisimamia kwa ukamilifu uhamasishaji wa michango ili kukamilisha mkakati huo.Waumini walichangia kwa moyo wa kupenda na kufanikisha mpango huo wa kuweka vigae (tiles) ndani ya Kanisa na Vitofali (paving blocks) katika maeneo yote ya nje ya kanisa na kuyabadilisha kabisa mandhali yote ya kanisa letu pia alihamasisha ujenzi wa shule ya ushonaji.

Upanuzi wa Kanisa

Baada ya uwekaji wa tiles na Paving Blocks Paroko Phocas Massawe alileta wazo la kupanua kanisa kwa sababu idadi ya waamini iliongzeka mara dufu.Halmashauri ya walei Parokia pamoja na waamini wote waliafiki wazo hilo.Lakini siyo tu kupanua Kanisa pia kuyaondoa mabati aina ya **Asbestors** ambayo ilibainika kuwa yanasumu na hayafai kiafya. Uhamasishaji wa kuchangia ulifanyika kwa waumini na kwa muitikio mkubwa waamini walianza kuchangia, mipango mingi ya kutafuta fedha ilitekelezwa na waumini wa Parokia hii. Kazi ya uchoraji wa Ramani

ulikamilika kwa wakati. Ramani hiyo ikakubaliwa michango iliendelea kwa kasi ili kutunisha mfuko wa upanuzi wa kanisa.

Ununuzi wa nyumba iliyo Jirani na Kanisa

Baada ya Ramani kukamilika ilionekana katika kupanua kanisa hili kutakuwa na shida kupitisha vifaa vya ujenzi ndipo wazo la kununua nyumba iliyojirani na kanisa lilipoibuliwa na Baba Paroko Phocas Massawe. Zile fedha zilizokuwa zimekusanywa kwa ajili ya kuanza upanuzi wa Kanisa, zilitumika kununulia hiyo nyumba. Ununuzi wa Nyumba hiyo kulichelewesha kwa muda wa kuanza upanuzi wa Kanisa. Waamini waliendelea kuchangia tena kwa moyo wa kupenda.

Katika kuimarisha Imani Katoliki kwa waumini na kuwajengea misingi Imara watoto wetu Padri Phocus Masawe alianzisha Misa na mafundisho ya dini dominika kwa watoto, watoto wengi waliibuliwa majumbani. Kabla ya mapano huu watoto waliokuwa wanafika kwenye Misa yao walikuwa si zaidi ya 300 na kwa sasa idadi hii imefikia 1500 ambapo hufika kwenye mafundisho ya dini Dominika (**Madido**) na baada ya mafundisho hayo huingia kanisani kwa Misa yao ambayo huanza saa 6.00. Pia

Uanzishwaji wa Kamati ya Uinjilishaji

Mwaka 2013 Pd. Phocas Massawe alianzisha kamati ya unjilishaji ya Parokia kwani kama kulitakiwa uinjilishaji kwenye Jumuiya ilibidi waazimwe wainjilishaji toka nje ya Parokia. Baba Pd Phocas Masawe kwa kushirikiana na wainjilishaJi walitembelea nyumba kwa nyumba kusimika Msalaba, Bibilia, Mshumaa na kubariki nyumba zote za waumini wa Parokia ya Mwananyamala

Mwaka 2014 Paroko Phocas Massawe alihamishwa na kuletwa Paroko mwingine ambaye ni **Padri Benedict Ndeyekiyo** ambae aliwahi kuwa Paroko wa Parokia hii miaka ya nyuma. Baba Paroko Benedict Ndeyekiyo

alipofika Parokiani aliendeleza yale yaliyoachwa na mtangulizi wake tena kwa kasi isiyo ya kawaida.

Paroko kutembelea nyumba za waamini wote wa Parokia

Baba Paroko Benedict Ndeyekiyo baada ya kuja na kuanza kazi ya utume katika Parokia yetu aliwatembelea majumbani mwao waamini wa parokia akibariki nyumba zao na kutoa ushauri mbalimbali kwa waamini ambao walikuwa hawajafunga ndoa na wenye vizuizi mbalimbali na ambao hawashiriki kwenye Jumuiya, hawaendi kanisani na kushiriki shuguli za maendeleo ya Parokia. Kazi hiyo ilichukua **muda wa Miezi Minne** kukamilisha kuwafikia waamini zaidi ya 12000 (Elfu kumi na Mbili).Zoezi hili liliamsha ari ya waamini kusali na kushiriki shughuli zote za maendeleo ya Parokia.

Uzinduzi wa Upanuzi wa kanisa

Baada ya kumaliza zoezi la kutembelea waumini kwenye jumuiya zote Baba Paroko kwa ushirikiano na Halmashauri ya Walei Parokia pamoja na waamini iliandaliwa siku maalumu ya Uzinduzi wa upanuzi wa Kanisa ambayo ilikuwa tarehe 1**5/08/2016**

Kauli mbiu aliyokuja nayo **Baba Paroko Benedct Ndeyekiyo ni Hii; Waamini wanatoa fedha zao bank na kuzileta kanisani halafu na sisi tunazirudisha bank tukisubiri ziwe nyingi.Kuanzia sasa fedha inayopatikana kwa ajili ya upanuzi wa Kanisa inapaswa zitumike mara moja,** waamini waliafiki mawazo mazuri ya Paroko na kazi ilifanyika kwa kasi kwa sababu iliwatia moyo waumini kwa kuona jinsi fedha zao zinavyotumika.Kazi ya ukarabati wa Kanisa ilikamilika kama ilivyokusudiwa.Waamini wameongezeka sana kusali siku za jumapili hata wale waamini waliokuwa wanasali sehemu zingine walirudi kwa maana Kanisa ni la Kiwango.Baadaye Paroko Msaidizi Padri Denis Ssebuffu alipata uhamisho akaletwa Paroko msaidizi mwingine Padri Apolinary Kibadeni.Mapadri hawa kwa kushirikiana na kamati

tendaji, Halmashauri ya Walei Parokia pamoja na waamini wanendelea na kazi ya umisionari ya kujenga Kanisa.

Maendeleo ya Kiroho yaliyopatiaka kuanzia kuanzishwa kwa Parokia

Tangu kuanzishwa kwa Parokia ya Mt Martin De Porres Mwananyamala mwaka 1971 ikiwa na idadi ya waamini 300 Parokia hii imepiga hatua kubwa kwa maendeleo ya kiroho.Imeweza kutoa Parokia tatu(3) ambazo ni Parokia ya Mwenge,Parokia ya Hananasifu na Parokia ya Mt. Yakobo Mtume Kijitonyama.

Pia imeweza kutoa **Mapdri saba (7)** wazawa wa Parokia ya Mt. Martin De Porres Mwananyamala ambao ni **Padri Paschal Bailon Libana, Padri Ladslaus Mikuza, Padri Joseph Mosha, Padri Sabath Mamboya, Padri Theofil Christopher Wabukundi, Padri Jeremiah Msaki na Padri David Ngate**.

Tuna **makatekista watano (5)** ambao wanatoa mafundisho ya Elimu ya dini kwa wanafunzi wakatoliki wa shule za msingi kumi (10) zilizo chini ya Parokia na kuwafundisha watoto wa Komunio ya kwanza, Ubatizo, Ndoa, Kipaimara na huduma zingine za Kanisa wanazopangiwa na Mapadri wetu.Na tunao **Masista wapato sita(6)** wanaotoa huduma mbalimbali kwa waumini wetu.

Kazi hii njema imefanikishwa na mapadri wetu kwa ushirikiano na Kamati tendaji, Halmashauri ya walei Parokia na waamini kwa ujumla.Wakristo wamekuwa mstari wa mbele kuunga mkono juhudi mbalimbali zilizokuwa zikifanywa na zinazofanywa na Mababa,Kamati Tendaji, Halmashauri ya Walei ili Injili ya Bwana wetu Yesu Kristo iweze kuhubiriwa kwa kila kiumbe.Mpaka sasa Parokia yetu ina jumla ya Kanda Kumi na mbili (12) ambazo ni

1. Kanda ya Mwanayamala Kisiwani "A" – ina Jumuiya nane (8)
2. Kanda ya mwananyamala Kisiwani "B" ina Jumuiya nane (8)

3. Kanda ya Victoria House ina Jumuiya tisa (9)
4. Kanda ya Kanisani Area ina Jumuiya saba (7)
5. Kanda ya Mwananyamala "A" ina Jumuiya Sita (6)
6. Kanda ya Mwananyamala "B" ina Jumuiya tano (5)
7. Kanda ya Mwananyamala "C" ina Jumuiya saba (7)
8. Kanda ya Makumbusho ina Jumuiya nne (4)
9. Kanda ya Kinondoni "A" ina Jumuiya tano (5)
10. Kanda ya Kinondoni "B" ina Jumuiya saba (7)
11. Kanda ya Kinondoni C"ina jumuiya saba (7)
12. Kanda ya Toplife ina Jumuiya tano (5)

- **Mpaka sasa idadi ya waumini kwenye parokia hii ni Elfu kumi na mbili na Mia nane kumi na mbili (12,812) Na Jumuiya Sabini na Tisa (79).**

Miradi ya maendeleo

Mradi uliopo nishule ya chekechea shule hii kwa mrefu inatoa huduma kwa watu wote bila upendeleo, na bila ubaguzi wa aina yeyote, miradi mingine ambayo ilishawahi kuwepo ni shule ya Useremala, na shule ya ushonaji miradi hii ilifungwa kwa sababu ilikuwa inaendeshwa kwa hasara.

Vyama vya Kitume

Kuna Vyama vya kitume mbalimbali katika Parokia hii ambavyo ni Wawata, Uwaka, Viwawa,Moyo Mtkatifu wa Yesu, Mtakatifu Anna, Almatea, Regio maria, Mtakatifu Vicent, Karismatic Katoliki, Wazee na Wastaafu na Wajane na Wagane vyama hivi vinafanya kazi kulingana na maelekezo ya Katiba zao.

Kamati Tendaji ya Kwanza tangu Parokia Kuanzishwa

Kamati tendaji ya kwanza kuhudumu katika Parokia ya Mt Martin De Porres Mwananyamala kuanzia Parokia kuanzishwa ni, **Mwenyekiti Raphael Mwanjali Makamu Mwenyekiti ,Marcus Mzalia, Katibu Eustace Tarimo,**

Katibu msaidizi ndugu Charles.Wenyeviti mbalimbali wa Kamati Tendaji waliohudumu kwa vipindi mbalimbali, **Marcus Mzania, Angels Liganga, Joseph Chonya, Severian Rwenyemani, Jackson Mbogha, Peter Msofe na Jeremiah Mchomvu.**

Viongozi wa sasa katika Parokia ya Mt De Porres Mwananyamala

- **Padri Benedict Ndeyekiyo – Paroko**
- **Padri Apolinary Kibadeni – Paroko Msaidizi**
- **Jeremiah Mchomvu – Mwenyekiti wa Kamati Tendaji**
- **Hilda Nyembo Makamu**
- **Emmanuel Makene – Katibu**
- **Elias R. Mpiga – Katibu Msaidizi**
- **Ateno Mosses - Mhazini**